KUSIKILIZA, KUZUNGUMZA NA KUSOMA - CBC GRADE 2 MID TERM 1 EXAMS 2023

SEHEMU YA 1:
SEHEMU YA A: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
<u>Mwalimu atamuuliza mwanafunzi maswali yafuatayo, mwanafunzi ayajibu vilivyo</u>

1. Hujambo?
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Maziwa ina rangi ipi?
   (Mwanafuzi ajibu)
3. Taja wanyama watatu wa porini.
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Mwalimu wako wa darasa anaitwa nani?
   (Mwanafuzi ajibu)
5. Chakula tunachokila asubuhi kina jina lipi?
   (Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU YA 2:
KUSOMA KWA SAUTI
<u>Soma hadithi hii kwa sauti</u>
Nilisikia watu wengi wakiongea nje. Nikatoka kuenda kuangalia. Nilimpata baba na mjomba wakiwa nje ya nyumba. Baba alimkaribisha mjomba sebuleni wakaketi kwa kiti cha sofa. Baada ya muda kidogo mama alikuja. Alimsalimia mjomba kisha akaingia ndani ya jikoni. Huko alitayarisha chai pamoja na mkate. Wakati tunakunywa chai mama alienda dukani kununua mchele. Aliporudi, alipi mchele ukawa wali. Mama pia alipika nyama. Chakula kile kilikuwa kitamu.